

**MKATABA WA KUUZIANA SHAMBA**

**MKATABA HUU UNAFANYIKA LEO HII TAREHE 27 MWEZI WA 11 MWAKA 2024.**

**KATI YA**

**Ndugu: MATIKO NYAMANG'O MUHORIA** wa Sanduku La Posta Namba 68 TARIME.  
Simu: 0766-534 303 na

**Ndugu: MWITA STEVEN WAIGAMA** wa Sanduku La Posta Namba 68 TARIME. Simu: 0763-914 086 (ambao kwa pamoja katika mkataba huu wataitwa "WAUZAJI" na atakapotajwa mmoja wao ataitwa "MUUZAJI" neno ambalo litahusisha wawakilishi wao au warithi wao wanaoweza ama kunufaika au kuwajibika kwa niaba yao kisheria) kwa upande mmoja.

**NA**

**SHAFRO INTERNATIONAL MINING COMPANY LTD**, Kampuni Iliyosajiliwa kwa Mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sanduku La Posta Namba 4071 DAR-ES-SALAAM. (ambayo katika mkataba huu itatajwa kama "MNUNUZI" neon ambalo litahusisha Kampuni yeyote ambayo itarithi mikoba ya kampuni hiyo (successor in title)) kwa upande wa pili..

**KWA KUWA: WAUZAJI** wanamiliki Kihalali SHAMBA Lenye ukubwa wa Ekari Kumi na Saba (17) lililopo katika Kijiji cha MURITO, Kitongoji cha MIRIMINSI, Kata ya KEMAMBO Wilaya ya TARIME VIJINI, Mkoa wa MARA, lililopo katika Leseni ya Uchimbaji Na. PML 0222MAR. (ambalo katika mkataba huu litaitwa "SHAMBA")

**KWA KUWA: WAUZAJI**, wakiwa na akili zao timamu, bila kushurutishwa na mtu yeyote yule, wapo tayari kumuuzia MNUNUZI SHAMBA hilo kwa makubaliano ya pesa taslimu, Shilingi Milioni Hamsini na mbili tu (Tshs 52,000,000/=) (ambazo katika mkataba huu zitaitwa "Bei ya Mauziano").

**KWA MAKUBALIANO HAYO, BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO:**

1. **KWAMBA: WAUZAJI** wameuza na MNUNUZI amenunua SHAMBA hilo kwa mujibu wa makubaliano na masharti yalitajwa katika mkataba huu.
2. **KWAMBA: WAUZAJI** wamemuuzia SHAMBA hilo MNUNUZI kwa ajili ya MNUNUZI kujenga Kiwanda cha Kuchakata Dhahabu (Gold Processing Plant (CIP)).
3. **KWAMBA: Bei ya Mauziano** imelipwa kwa awamu moja, yaani MNUNUZI amelipa na WAUZAJI wamepokea Pesa taslimu Shilingi Milioni hamsini na mbili tu (Tshs 52,000,000/=) leo hii tarehe 27 mwezi wa 11 mwaka 2024 ikiwa ni malipo kamili ya Bei ya Mauziano. MATIKO



4. **KWAMBA: WAUZAJI** wanathibitisha kwamba wamecuza **SHAMBA** walilokuwa wakilimiliki kihalali wao wenyewe bila mshirika wala mmiliki mwenza mwingine wa aina yoyote ile, na kwamba **SHAMBA** hilo halina deni wala madai mengine yoyote yale.
5. **KWAMBA: WAUZAJI** wanathibitisha kuwa yote waliyoyaeleza kuhusiana na **SHAMBA** hilo ni ya kweli kabisa na wana ahidi kumfidia **MNUNUZI** kikamilifu endapo itatokea kesi ya madai, ya jinai au madai mengine yoyote yatakayo tokana na **WAUZAJI** kutokueleza ukweli katika yale waliyoyathibitisha katika Mkataba huu.
6. **KWAMBA: MNUNUZI** naye anathibitisha yafuatayo:
  - a) Analifahamu **SHAMBA** hilo na amelikagua na kuridhika nalo kabla ya kufanya mkataba huu.
  - b) Hatakuwa na madai mengine yoyote kuhusu **SHAMBA** hilo mara baada ya kutia sahihi mkataba huu.
7. **KWAMBA:** Pande Mbili za Mkataba huu zimekubaliana kwamba **WAUZAJI** wanawajibika kukabidhi **SHAMBA** hilo kwa **MNUNUZI** leo hii tarehe 27 mwezi wa 11 mwaka 2024.
8. **KWAMBA:** Mkataba huu utawabana Warithi na Wawakilishi wa aina yoyote ile wa Pande Mbili za Mkataba huu ambao wanaweza ama kunufaika au kuwajibika kwa niaba ya Pande Mbili za Mkataba huu.

**KWA USHAHIDI HUU BASI:** Pande mbili zinatia sahihi zao siku na mwezi kama inavyoonekana hapa chini

**IMESAINIWA NA: MATIKO NYAMANG'O MUHORIA**  
ambaye ninamfahamu binafsi/ nimetambulishwa kwake na

.....

ambaye ninamfahamu binafsi, hapa Kahama, leo hii

tarehe 27 mwezi 11 mwaka 2024

**MUUZAJI**

**IMESAINIWA NA: MWITA STEVEN WAIGAMA**

ambaye ninamfahamu binafsi/ nimetambulishwa kwake na

.....

ambaye ninamfahamu binafsi, hapa Kahama, leo hii

tarehe 27 mwezi 11 mwaka 2024

**MUUZAJI**

MATIKO

Shahidi: 1. JINA: MATIYO NYAMANGA MUHOZIA SAHIHI: MATIYO  
2. JINA: MARIYA STEVEN WAKWAMA SAHIHI: HHS

**MBELE YANGU:**

JINA: SIRAJI MUSSA KWIKIMA

SAHIHI: [Signature]

WADHIFA: WAKILI

ANWANI: S.L.P 280 TABORA



**IMESAINIWA NA:** IMESAINIWA NA KUGONGWA

**MUHURI WA SHAFRO INTERNATIONAL MINING**

COMPANY LTD, hapa Mara, mbele yangu, leo hii tarehe 27 mwezi 11 mwaka 2024



JINA: HUSSEIN KWIKIMA

WADHIFA: MURUGENI

SAHIHI: [Signature]

JINA: SHANAVAS EDATHIL

WADHIFA: MURUGENI

SAHIHI: [Signature]

**MBELE YANGU:**

JINA: SIRAJI MUSSA KWIKIMA

SAHIHI: [Signature]

WADHIFA: WAKILI

ANWANI: S.L.P 280 TABORA



**IMEANDALIWA NA:**

**SIRAJI MUSSA KWIKIMA, WAKILI**

**KIWANJA Na. 179 Kitalu "E"**

**Boma Road.**

**Kahama**

**S.L.P 280 Tabora**

**Simu: 0753 – 214 547**

**Email: [sirajimlela@gmail.com](mailto:sirajimlela@gmail.com)**